Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 3 Issue 1 | [December] [2026] | [Page 95] – [Page 123]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

Maneno Mnasaba Na Sauti Mrejeo Katika Kitumbatu Na Kimakunduchi

Zainab Ali Iddi

Department of Kiswahili, The State University of Zanzibar, Tanzania
Corresponding Email: zainab.iddi@suza.ac.tz

Article History:
Received: June 1, 2026
Accepted: July 15, 2026
Online First: November, 25, 2026

Keywords: Sauti mrejeo, Maneno mnasaba, Kimakunduchi na Kitumbatu.

This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license

Ikisiri

Makala hii inaangazia maneno mnasaba na sauti mrejeo katika Kitumbatu na Kimakunduchi. Katika maneno ya lugha, kuna sauti ambazo hutafautiana kimaumbo lakini sauti hizo hazibadilishi maana. Kwa mfano, katika Kiswahili maneno 'mgahawa' na 'mkahawa' yanatofautiana kwa sauti /g/ na /k/ licha ya tafauti hizo maneno hayo yana maana sawa. Data za makala hii zinatokana na utafiti wangu wa Uzamivu (2018). Data hizo zimekusanywa kupitia njia ya mahojiano, dodoso na ushuhudiaji. Nadharia ya Isimu-historia na Linganishi ikitiwa mwega na mbinu linganishi imetumika kuongoza uwasilishaji na uchambuzi wa data. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kwamba kuna sauti mrejeo katika lahaja hizi zilizokitwa na mfanano wa sifa za sauti hizo. Sauti hizo ni [t] na [tʃ], [w] na [y], [p] na [v], [d] na [l], [k] na [y], [py] na [t], [g] na [ng], [p] na [v], [ʌ] na [a,o, u]. Katika muktadha huo, tunabaini kwamba lahaja za Kimakunduchi na Kitumbatu zina asili moja kwa maana kwamba lahaja hizi zinatokana na mame-lugha moja. Aidha, sauti mrejeo zilizojitokeza zinaweza kupatikana katika lugha au lahaja nyingine kwenye mazingira sawa na yaliyojitokeza katika Kitumbatu na Kimakunduchi. Makala yamebaini kuwa bado mjadala zaidi unahitajika kuhusiana na

sauti mrejeo katika lahaja na lugha nyingine za Kibantu na Afrika kwa ujumla ili kuweza kuelewa kwa kina maneno mnasaba baina ya lugha mbalimbali.

Abstract

This article examines cognate words and correspondence sounds in Kitumbatu and Kimakunduchi. In language, there are sounds that differ in their phonetic realization but do not result in a change of meaning. For example, in Swahili, the words mgahawa and mkahawa differ only in the sounds /g/ and /k/; despite this difference, they convey the same meaning. The data presented in this article are drawn from my PhD research Thesis (2018). Data were collected through interviews, questionnaires, and participant observation. The Historical-Comparative Linguistic Theory, supported by the Comparative Method, was employed to guide the presentation and analysis of the data. The findings reveal the existence of correspondence sounds in these dialects, established on the basis of shared phonetic features. The identified correspondence sounds include [t] and [tʃ], [w] and [y], [p] and [v], [d] and [l], [k] and [y], [py] and [t], [g] and [ng], [p] and [v], and [ʌ] and [a, o, u]. These findings suggest that the Kimakunduchi and Kitumbatu dialects share a common origin, indicating that they are derived from the same proto-language. Furthermore, the correspondence sounds identified in this study may also occur in other languages or dialects under phonological environments similar to those observed in Kitumbatu and Kimakunduchi. The article concludes that further investigation of correspondence sounds in other Bantu languages and dialects, as well as African languages more broadly, is necessary to enhance our understanding of cognate words across languages.

Utangulizi

Makala hii inachunguza maneno mnasaba katika lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Makala imeangazia maneno hayo ili kudhirisha zaidi uhusiano uliopo baina ya lahaja hizo mbili jambo ambalo litasaidia kubaini tafauti na mfanano wa maneno mnasaba katika lahaja hizo.

Maneno mnasaba na sauti mrejeo ni miongoni mwa kidhibiti thabiti cha kutoa ushahidi unaobainisha uhusiano wa asili wa kinasaba wa lugha (Kondrak, 2019). Maelezo ya Kondrak yanatubainishia kuwa hii ni njia bora katika kubaini historia ya lugha pamoja na mamelugha za asili za lugha mbalimbali. Akifafanua zaidi, Kondrak anasema kuwa hapo awali, karibu

miaka mia mbili iliyopita, wanaisimu wa Kihistoria wamekuwa wakitumia mbinu linganishi kwa kuangalia mfanano wa msamiati wa msingi. Baada ya muda kupita, mwelekeo ulibadilika na hivyo kuhusisha jozi za maneno na kuangalia sauti mrejeo katika maneo hayo ili kubaini maneno mnasaba ambayo huonesha uhusiano wa kinasaba uliopo baina ya lugha na lugha nyingine au lahaja. Kwa kutumia njia hii, Kondrak anadai kuwa wataalamu waliweza kubaini chanzo cha asili cha lugha za Ulaya na Bara Hindi. Hata hivyo uchunguzi kama huu kwa lugha ya Kiswahili bado haujafanyika na hivyo kuacha pengo la kitaaluma hasa katika uwanja wa isimu. Kwa muktadha huu, makala hii imekusudia kuziba pengo hilo kupitia utafiti wa kiulingnishi wa Kitumbatu na Kimakunduchi.

Wataalamu mbalimbali wameelezea maneno mnasaba, baadhi yao ni Hornby (2005), De Groot (2011), Frunza (2016) na Kondrak (2019). Hata hivyo, katika makala hii maneno mnasaba yameangaliwa kwa kutumia mtazamo wa Kondrak (2019) ambapo ameainisha maneno mnasaba kwa kutumia vigezo vitatu; navyo ni sauti mrejeo, mfanano wa kifonetiki na mfanano wa Kimaana. Makala hii imebainisha maneno mnasaba kwa kujiegemeza na mtazamo wa Kondrak kwa kutumia vipengele viwili kati ya vitatu navyo ni: kipengele cha Sauti mrejeo; na Mfanano wa Kimaana. Sababu za kujiegemeza katika mtazamo wa Kondrak na kuteua vigezo hivi ni kwamba vinaweza kutambua uhusiano wa asili uliopo baina ya sauti au jozi za maneno ya lugha au lahaja tafauti ambazo zinaaminika kuwa zinatoka katika asili na mamelugha moja. Kama kwamba haitoshi, mara nyingi hapo awali, lugha ziliwekwa katika familia kutokana na kufanana kwa msamiati wa msingi. Kinyume na hayo, baadaye mfanano wa sauti ulipewa kipaumbele na kuchukuliwa kama ushahidi wenye nguvu katika kubaini uhusiano wa kinasaba wa maneno uliopo.

Hapana shaka, muktadha huu huweza kubainisha kwa uwazi kabisa uhusiano wa kihistoria uliopo kama ni wa kinasaba au kinyume chake. Katika kuhakikisha na kupata uthabiti wa maneno mnasaba, Kondrak anadai kuwa maneno ya mkopo hayafai kulinganishwa. Makala imeteua lahaja mbili hizi kutokana na kuaminika kuwa zinatokana na mamelugha moja. Katika utafiti wake Juma (2019:99) alilinganisha Kitumbatu na Kimakunduchi na ili kubaini jinsi zinavyofanana na kutofautiana. Matokeo yanaonesha kuwa hizo ni lahaja mbili tofauti za lugha moja. Akifafanua zaidi

Juma (2019: 223) anasema kuwa mfanano huo unatokana na ukweli kwamba lahaja hizi zina uhusiano wa kimnasaba, hivyo tofauti ndogo ndogo zinazojitokeza husababishwa na mwachano wa lahaja hizi kijiografia. Hoja ya Juma inashadididiwa pia na Juma (2012), Iddi (2012) na Iddi (2018).

Kwa vile maneno mnasaba hubainishwa kupitia lugha mbili au zaidi, ni wazi kuwa katika kila lugha au lahaja maana huweza kuelezwa kwa kutumia maneno tafauti ambayo kwa kiasi hulingana na kukaribiana kimaana ama kwa ukaribu au kiumbali. Makala hii imeainisha maneno mnasaba kutoka Kitumbatu na Kimakunduchi yenye maana zinazolingana kwa kuyagawa katika sehemu tatu; maneno mnasaba yenye maana moja lakini umbo tafauti, maneno mnasaba yenye umbo moja na maneno mnasaba yenye kutafautiana kimatamshi kupitia sauti zinazorejeana. Aidha maneno ya kigeni au ya mkopo hayawezi kupewa sifa ya maneno mnasaba (Kondrak 2019).

1.1 Maneno Mnasaba

Dhana ya maneno mnasaba imeelezwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwao ni Hornby (2005) anasema kuwa neno mnasaba ni neno lenye chanzo kimoja au asili moja na neno jingine.

Frunza (2006) anasema kwamba maneno mnasaba ni yale yenye kufanana kimaana ambapo neno moja huweza kuwa kama jozi maana ya mwenziwe ijapokuwa kuna tafauti ya kiotografia. Hivyo basi, maneno mnasaba ni maneno yenye asili na chimbuko moja ambapo huweza kufanana kiumbo, kimaana na kiotografia au yakatafautiana kimatamshi lakini yakawa na maana sawa.

TUKI (2009) nao wanatoa ufafanuzi kuwa katika Isimu Linganishi na Isimu Historia, maneno mnasaba ni upatanisho uliopo baina ya maneno au miundo iliyo na uhusiano wa kiasili ingawa miundo hiyo inaweza kuwa na sura au maumbo yasiyofanana katika umbo lake la nje.

De Groot (2011) anafafanua unasaba wa maneno kupitia mtazamo wa kitamaduni ambao huibuka na kujitokeza zaidi kunapokuwa na tafauti katika viwango vya maana.

Kwa upande mwengine, Kondrak (2009) anaeleza kuwa maneno yenye asili moja ambayo yamo katika lugha tofauti yenye mfanano wa sauti unaojirudia katika orodha za maneno hujulikana kama maneno mnasaba.

Akifafanua zaidi anasema kuwa maneno mnasaba ni kipengele cha msingi katika isimu historia ambapo kina kazi mbili za msingi nazo ni kuonyesha uhusiano wa lugha zenye asili moja na kujenga upya historia za familia za lugha. Hivyo, maneno mnasaba ni kiashiria muhimu kinachoweza kutoa ushahidi thabiti wa lugha zenye asili moja ambapo lengo kuu ni kusaidia wanaisimu wa kihistoria kuthibitisha uhusiano wa lugha.

Maelezo karibu yote ya wataalamu yanakubaliana kuwa maneno mnasaba hutokana na asili moja na hivyo huweza kufanana au kutafautiana lakini maana zinalingana. Kwa muktadha huu, tunaweza kusema kuwa maneno mnasaba ni yale yenye kufanana kimatamshi, kimuundo na kimaana jambo ambalo linadhirisha kuwa maneno mnasaba ni maneno yenye asili na chimbuko moja. Pia kwa upande mwengine, maneno hayo huweza kufanana au kutafautiana kiumbo na kiotografia lakini yakawa na maana sawa.

Aidha, kama tulivyoeleza awali kuwa moja katika kipengele cha kubainisha maneno mnasaba ni sauti mrejeo, hivyo basi ni vyema tukaielewa dhana hiyo.

1.2 Sauti Mrejeo

Dhana ya sauti mrejeo inaelezwa na Massamba (2016) kuwa katika taaluma ya isimu-historia na linganishi, ni sauti zinazorejeana katika maneno ambayo hujulikana kama maneno mnasaba. Hivyo, sauti mrejeo ni sauti ambazo hurejelea kitu kilekile kimoja katika maneno hata kama sauti hizo zinatofautiana kimaumbo

Sauti mrejeo zinachukua nafasi muhimu sana katika uainishaji wa uhusiano wa nasaba katika lugha. Wanaisimu hutumia sauti mrejeo ili kuweza kubainisha uhusiano wa asili wa lugha katika kuunda maumbo yenye mamelugha moja na kwa ajili ya ujiundaji upya wa familia mnasaba ya zamani inayokitwa katika uvumbuzi wa kushirikiana Kondrak (2019).

Mara nyingi, imezoeleka kwamba tunapojadili mabadiliko ya sauti katika neno sauti hizo huhusishwa na michakato ya kifonolojia au kimofofonolojia. Kinyume na hali hiyo sauti mrejeo hazitegemei michakato hiyo bali hutokea kiunasibu tu katika familia za lugha. Kwa upande mwengine, kuna uwezekano mkubwa kwa sauti iliyomo kwenye lugha moja isiwemo katika mfumo wa sauti wa lugha nyengine na hivyo kusababisha neno hilo kutumia sauti nyingine ama inayofanana kimatamshi au

inayokaribiana katika pahala pa kutamkia jambo linalosababisha sauti kurejeana

Ifahamike kwamba muktadha wa sauti mrejeo hutokea pale ambapo mabadiliko ya sauti hujitokeza kwa sauti moja huchukua nafasi ya sauti nyingine bila ya kubadili maana katika neno. Hata hivyo mabadiliko hayo hayatokei kwa bahati mbaya tu bali husukumwa na sababu tafauti (Clackson 2007).

Mosi, mazoea katika jamii kutokana miiko iliyopo. Kila jamii huwa na maneno ambayo ni karaha na hayaruhusiwi kutamkwa hadharani. Katika kuhakikisha miiko ya jamii hiyo haikiukwi neno hilo hupokea mabadiliko na kutamkwa vingine ambapo ama sauti huachwa au kubadilika. Kuepukwa kwa utamkaji wa sauti ya asili katika neno husababisha kuibuka kwa sauti nyingine na hivyo kuchukua nafasi ya sauti ya awali.

Pili, Ukopaji au utohowaji wa neno kutoka lugha moja kwenda nyingine husababisha kupatikana kwa sauti mrejeo. Hii ni kwa sababu neno linapotoholewa mara nyingi hufuata mfumo wa sauti wa lugha iliyokopa jambo linalosababisha pengine kupotea kwa uasili wa sauti ya awali au hata upokeaji wa sauti usio sahihi wa neno hilo kutokana na mazoea ya lugha.

Akitilia mkazo hoja hiyo Clackson (2007) anadai kwamba kila lugha ina mfumo wake wa sauti ambapo idadi na aina ya sauti hutofautiana kutoka lugha moja na nyingine. Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa kwa sauti iliyomo kwenye neno lililokopwa isiwemo katika mfumo wa sauti wa lugha hiyo na hivyo kusababisha neno hilo kutumia sauti nyingine ama inayofanana kimatamshi au inayokaribiana katika pahala inapotamkwa jambo linalosababisha sauti mrejeo kama anavyobainisha katika utafiti wake wa sauti mrejeo baina ya lugha ya Kiingereza na Kijerumani ambapo sauti th [θ] na [t] katika Kiingereza hujitokeza kama sauti [d], na [z] na [ʧ] kwenye Kijerumani. Zingatia mifano kama ifuatayo:

Kiingereza	**Kijerumani**	**Kiingereza**
Thorn	dorn	Thorn
toe	zeh	toe
tooth	zahn	tooth

Muktadha huu pia unajitokeza katika Kitumbatu na Kimakunduchi ambapo katika lahaja hizo hakuna sauti /ð/, /ɣ/, /θ/na /χ/ badala yake hutumia sauti zinazorejeana /z/, /gh/, /s/ na /h/ (taz. Iddi 2012 na 2018). Hii ni kutokana na kama alivyoeleza Clackson kuwa baadhi ya sauti hasa kupitia maneno ya mkopo huweza kukosekana kama inavyojionesha katika mfano ufuatao:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
ðambi	zambi	zambi
ɣaðabu	hazabu	hazabu
θamani	samani	samani
χamis	hamis	hamis

Kwa jumla, sauti mrejeo zinachukua nafasi muhimu sana ambapo Wanaisimu hutumia sauti mrejeo ili kuweza kubainisha uhusiano wa asili wa lugha na kwa ajili ya ujiundaji upya wa familia mnasaba ya zamani inayokitwa katika uvumbuzi wa kushirikiana.

Mapitio ya Kazi Tangulizi

Kama tulivyobainisha awali kuwa maneno mnasaba yamechunguzwa na wataalamu kupitia tafiti za lugha mbalimbali. Hata hivyo mtafiti wa makala hii hakuweza kubaini andiko linalohusiana na maneno mnasaba katika lahaja za Kitumbatu na Kimakunduchi.

Katika utafiti wake, Frunza (2006) na anaeleza kuwa maneno mnasaba ni jozi za maneno yanayofanana kiotografia na kuwa na tafauti hata ndogo katika matamshi huchukuliwa kama maneno tu yanayokaribia kuwa mnasaba. Maelezo ya wataalamu hawa yanaungana na mitazamo ya wataalamu wengine wanaodai kuwepo kwa maneno mnasaba bahatishi. Hata hivyo makala hii haikugusia wala kuzungumzia maneno mnasaba bahatishi.

Kondrak (2019) katika utafiti wake anaeleza maneno mnasaba kuwa ni maneno yanayofanana, ambayo etimolojia yake ni ya asili moja. Hata hivyo, baada ya muda mrefu kupita matamshi huweza kubadilika.

Mabadiliko hayo huweza kusababishwa na mambo mbalimbali kama vile mabadiliko katika mazingira ya kifonetiki na mawasiliano ya lugha na kanuni za lugha. Katika kuthibitisha maelezo yake Kondrak alibainisha mfano kutoka lugha ya Kiingereza na Kijerumani kwa neno "*night*" (Kiingereza) na "*nacht*" (Kijerumani) kwa kubainisha kuwa haya ni maneno yanayofanana, lakini matamshi yao yamebadilika sana baada ya karne nyingi. Utafiti wa Kondrak umesaidia sana kutoa mwanga namna matamshi yanavyobadilika katika maneno jambo ambalo limezungumziwa katika makala hii.

List, Greenhill na Gray (2017) walifanya utafiti wa kuchunguza maneno mnasaba kwa kulinganisha maneno kwa kutumia mbinu ya kiotomatiki. Mbinu hiyo ilitumia kompyuta ambapo watafiti hawa wanasema kwamba njia hii ni muhimu katika uchunguzi wa uhusiano wa maneno ya asili ili kubaini historia ya maneno hayo hasa pale ambapo ushahidi wa kihistoria haupo au ni mdogo. Mtazamo huu ulikuja kuungwa mkono na Batsuren, Bella, & Giunchiglia (2021) ambapo nao walifanya tafiti kuhusu maneno mnasaba kwa kutumia mbinu za kihistoria na kompyuta. Kupitia utafiti wao waliweza kuchunguza maneno mnasaba yenye asili moja kutoka lugha zaidi ya mia tatu. Ni dhahiri kwamba, katika kuchunguza asili na historia ya maneno data zenye mawanda mapana ni muhimu kwa vile husaidia kutambua maneno yenye asili moja kwa usahihi (taz. Kondrak 2019 na Greenberg 1993).

Utafiti wa List na wenzake (2017) umetoa mwanga kwa utafiti huu katika kubaini asili na chimbuko la lugha mbalimbali zenye muwasala mmoja na zinazotokana na mamelugha moja kwa kutumia njia za ulinganishi tafauti tafauti. Hata hivyo, utafiti wa List na wenzake (2017) umetafautiana na utafiti huu kupitia njia zilizotumika katika kulinganisha lugha hizo ili kupata sauti mrejeo ambazo zinasababisha maneno mnasaba. Hii ni kwan sababu List na wenzake (2017) wametumia mbinu ya Kiotomatiki kinyume na utafiti wa makala hii ambao umetumia sauti mrejeo na mlingano wa kimaana bila kuhusisha mbinu ya kiotomatiki.

Kwa upande mwengine, tafiti za miradi ya awali za Dyen, Kruskal, na Black (1992) zilihifadhi lugha za Kihindi-Ulaya (Indo-European) na kuwa

kama kiolezo faridi na hivyo kuweka msingi imara wa kulinganisha maneno pamoja na kuendeleza tafiti za baadaye. Ingawa wataalamu hao katika utafiti wao hawakutumia teknolojia ya kisasa ya kompyuta katika kuchanganua data kama alivyofanya Kondrak lakini ulitoa mchango muhimu katika kuonesha uwezekano wa kuunda na kukusanya data nyingi za takwimu za kileksia ambapo hulinganisha lugha kwa kutumia takwimu za msamiati wenye kujitokeza mara nyingi huonekana kuwa na uhusiano wa kinasaba.

Tafiti za wataalamu hawa zimetoa mwanga wa uchunguzi wa kuweza kuunganisha mbinu za kihistoria, kompyuta na kisaikolojia katika uainishaji na uelewa wa maneno mnasaba.

Igoa na wenzake (1992) walichunguza maneno mnasaba katika lugha ya Kihispania na Kiingereza. Katika utafiti wao walibainisha aina tatu za uhusiano wa maneno yenye unasaba nazo ni; kwanza, maneno yanayofanana kimaumbo na kimaana. Mfano neno *festival* ambapo katika lugha zote mbili Kihispania na Kiingereza neno hilo lina maana ya sherehe. Pili maneno yenye maana sawa lakini yana tafauti ndogo za kimatamshi, mfano *observacion* (Kihispania) na *observation* (Kiingereza). Aina ya tatu ni maneno mnasaba ya kibahati ambayo yanafana kimaana na kutofautiana kimaumbo. Igoa na wenzake walitoa mfano wa maneno hayo kama vile *libro* na *panaderia* (Kihispania) *book* na *bakery* (Kiingereza).

Mapitio ya maandiko yaliyopitiwa katika makala hii yamebaini kuwa lugha zilizochunguzwa na kufafanuliwa kuhusiana na maneno mnasaba ni Kiingereza, Kijerumani na Kihindi – Ulaya kinyume na utafiti huu ambao umeangalia lahaja za Kiswahili; Kitumbatu na Kimakunduchi. Ifahamike kwamba kuna mwachano mkubwa wa kijiografia, chanzo na chimbuko baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi na lugha zilizofanyiwa mapitio.

Aidha, pamoja na mchango mkubwa wa wataalamu hao, bado kuna tafauti ya matumizi ya mbinu za uchambuzi ambapo baadhi yao wametumia mbinu za kiotomatiki na utafiti huu umetumia mbinu linganishi kwa kuangalia sauti mrejeo na maana. Pia tafiti hizo zimejikita katika baadhi tu ya sauti ili kuona maneno mnasaba kinyume na utafiti huu ambao umechambua kwa kina sauti mrejeo katika Kitumbatu na Kimakunduchi ili kubaini maneno mnasaba. Hali hii imechangia kuwepo kwa pengo la kitaaluma ambalo makala hii imelichunguza na kutoa ufafanuzi juu ya

muwasala wa lahaja hizo za Kiswahili.

2.1 Mapitio kuhusu Sauti Mrejeo

Kwa ujumla, sauti mrejeo zimezungumziwa katika lugha mbalimbali ulimwenguni hususan lugha za Ulaya na Bara Hindi. Mfano, Clackson (2007) alichunguza sauti mrejeo katika lugha kumi na moja (11) za Kihindi – Ulaya *(Indo Eropean languages)*. Katika utafiti wake alichunguza vipasuo vikwamizi namna vinavyorejeana. Utafiti wa Clackson ni muhimu kwa makala hii kwa vile umezungumzia sauti zinavyorejeana ijapokuwa umejikita katika sauti maalumu; vipasuo vikwamizi tu. Pia umeachana na makala hii kwa vile sauti zilizochunguzwa ni kutoka Kihindi–Ulaya ambazo zinatafautiana na Kitumbatu na Kimakunduchi.

Naye Kroonen (2013) aliangalia sauti mrejeo katika lugha za Kijerumani, Kidachi na Kiingereza na kushughulikia sauti tatu tu nazo ni [θ, t, d] ambapo alibaini kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya sauti hizo unaotokana na uasili wa sauti za lugha hizo. Kwa mfano *heart* na *foot* (Kiingereza), *kord na ped* (Kidachi). Sauti hizi pia zimechunguzwa katika makala hii na hivyo kusaidia katika uchambuzi wake ijapokuwa kuna tafauti namna zinavyotumika katika lugha hizo na lahaja zinazochunguzwa.

Kwa upande mwengine, Brown, Holman na Wichman (2013) wamefafanua sauti mrejeo katika muktadha wa sauti mwambatano. Katika maelezo yao wanasema kuwa kwenye sauti hizo kuna mpangilio maalumu wa ujitokezaji ambapo sauti hujitokeza kama ulivyo utaratibu na mpangilio wake kwenye matamshi; konsonanti za mbele au zilizo juu hutangulia na kufuatiwa na konsonanti za nyuma. Katika uchunguzi wao baadhi ya sauti walizobainisha ni sauti mrejeo mwambatano za nazali /ᵐb/ na /ɲ/.

Meillet (1908) anaeleza kwamba moyo wa Isimu-historia sio ujiundaji upya kiisimu, bali ni ukweli unaobainika au uliopo katika ruwaza za mrejeo. Akisisitiza zaidi anaeleza kuwa ujiundaji upya si chochote bali ni alama ya kile tunachokiita mrejeo kwa umbo fupi. Hoja ya Meillet inatuonesha umuhimu wa sauti mrejeo katika lugha. Kwa ujumla, tafiti zilizoangalia sauti mrejeo zaidi zimezungumzia sauti katika lugha za Ulaya na Bara Hindi ilhali utafiti huu umejikita katika lahaja za Kiswahili; Kitumbatu na Kimakunduchi.

2.3 Mkabala wa Kinadharia

Makala hii imetumia nadharia ya Isimu-historia na Linganishi iliyoanzishwa na William Jones (1786). Nadharia hii hutumika ili kulinganisha na kulinganua lugha au lahaja katika muktadha wa kihistoria na kuhusiana kwake na hivyo kubainisha kufanana na kutofautiana. Ifahamike kwamba, mbinu linganishi imesaidia sana kubainisha lugha nyingi ulimwenguni ambazo zimehusiana. Makala imeamua kutumia nadharia hii kwa kuona inafaa katika uchambuzi wa data za makala hii katika kubainisha mnasaba wa sauti zinazorejeleana baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi.

Kwa upande mwingine, nadharia hii huweza kuchunguza historia ya maendeleo ya lugha katika kipindi mahsusi, cha nyuma, nyuma sana, cha kati au cha karibuni. Kwa ujumla, ili kuweza kuzilinganisha lugha/lahaja mbili au zaidi na kubaini uhusiano wake katika vipengele mbalimbali vya lugha wanaisimu hutumia mbinu linganishi ambayo ndiyo msingi wa nadharia hii. Anttila (1972) anaeleza kwamba mbinu linganishi hutumiwa katika isimu linganishi ili kuchambua lugha zenye asili moja na kuweza kubainisha uhusiano wake wa asili.

Mbinu linganishi huweza kuchunguza na kubainisha mfanano na tofauti katika mfumo wa maumbo ya maneno (mofolojia), miundo ya maneno (sintaksia), mfumo wa uainishaji wa nomino (ngeli) kwa kutaja baadhi. Kwa vile lengo la makala hii ni kuchunguza sauti mrejeo katika Kitumbatu na Kimakunduchi, katika uchambuzi wake wa data, kigezo cha kuchunguza sauti kwenye maneno mbalimbali yenye maana moja kimetumika.

Vile vile mbinu linganishi huweza kutumia visawe kwa kuangalia kama lugha hizo zina visawe sawa au vinatofautiana. Visawe hivyo huweza kubainisha kama maneno hayo yana maana sawa na sauti sawa au maana sawa lakini yana sauti zinazotafautiana. Mfano, visawe kutoka katika lugha/lahaja mbili au zaidi huweza kuwa na maana sawa lakini baadhi ya sauti zikatafautiana

Hivyo basi, lengo la makala hii ni kuangalia maneno mnasaba na sauti mrejeo katika Kimakunduchi na Kitumbatu. Aidha, Nadharia ya Isimu-Historia na Linganishi imesaidia kuweka bayana mfanano na tafauti zilizopo baina ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu kwenye muktadha wa maneno mnasaba na kuweza kubainisha muwasala wa kinasaba baina yao.

Methodolojia

Makala hii imetumia mkabala wa kitaamuli wenye muundo wa kimaelezo na linganishi katika kuchunguza maneno mnasaba na sauti mrejeo katika lahaja za Kitumbatu na Kimakunduchi. Data zilizotumika zimetokana na utafiti wa uzamivu uliofanywa na mtafiti mwaka 2018. Mkabala huu ulifaa kwa sababu uliwezesha kukusanya, kueleza na kulinganisha msamiati wa lahaja hizo mbili kwa kuzingatia maumbo ya maneno, matamshi, maana na mazingira ya ujitokezaji wa sauti. Kitumbatu na Kimakunduchi ziliteuliwa kutokana na kuwa lahaja za Kiswahili zinazodhaniwa kuwa na uhusiano wa kinasaba na chimbuko la pamoja.

Data zilikusanywa kutoka kwa wazungumzaji wa lahaja hizo kwa kutumia mahojiano, dodoso na ushuhudiaji shirikishi. Mahojiano yalisaidia kupata maneno yanayotumika katika mawasiliano ya kawaida pamoja na maelezo kuhusu maana na matamshi yake. Dodoso lilitumika kukusanya msamiati unaolingana kutoka katika lahaja zote mbili kwa utaratibu unaorahisisha ulinganishaji. Ushuhudiaji shirikishi ulimwezesha mtafiti kusikiliza matumizi halisi ya lahaja hizo katika mazingira ya mawasiliano na kuthibitisha matamshi ya maneno yaliyopatikana kupitia mbinu nyengine. Matumizi ya mbinu zaidi ya moja yalisaidia kulinganisha data na kuimarisha uthabiti wa matokeo.

Uchambuzi uliongozwa na Nadharia ya Isimu-Historia na Linganishi iliyoasisiwa na William Jones (1786), ikisaidiwa na mbinu linganishi. Maneno ya Kitumbatu na Kimakunduchi yaliwekwa katika jozi na kuchunguzwa kwa kuzingatia vigezo viwili vilivyotokana na mtazamo wa Kondrak: sauti mrejeo na mlingano wa kimaana. Msamiati wa msingi ulipewa kipaumbele kwa sababu huwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi sifa za kihistoria za lugha. Maneno ya mkopo yaliondolewa katika uchambuzi ili yasitoe taswira isiyo sahihi kuhusu uhusiano wa kinasaba wa lahaja hizo.

Data zilipangwa katika makundi matatu: maneno yenye maumbo sawa na maana sawa; maneno yenye maumbo tofauti lakini maana sawa; na maneno yanayotofautiana kimatamshi kutokana na sauti mrejeo bila

kubadilika kwa maana. Jozi za maneno zililinganishwa ili kubaini sauti zinazojirudia katika mazingira yanayofanana. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na majadwali yanayoonesha maneno ya Kiswahili Sanifu, Kitumbatu na Kimakunduchi. Utaratibu huu uliwezesha kubainisha mfanano, tofauti na uhusiano wa kihistoria wa lahaja hizo.

Matokeo na Mjadala

Kama tulivyoeleza awali kuwa uchambuzi wa maneno mnasaba umejiegemeza kwa kutumia mtazamo wa Kondrak 2019 ambapo aliangalia sauti mrejeo, mfanano wa kifonetiki na uhusiano wa kimaana. Aidha kwa kutumia sauti mrejeo na maneno mnasaba katika Kitumbatu na Kimakunduchi uchambuzi wa makala hii umegaiwa katika makundi mawili. Kwanza, kundi la maneno mnasaba yanayotafautiana kiumbo lakini maana zao sawa na kundi la pili ni la maneno mnasaba kwa kigezo cha sauti mrejeo lakini maana zake ni sawa.

Maneno Yanayotafautiana Kimatamshi

Kama tulivyokwishaeleza hapo awali kuwa Lugha zinazohusiana kinasaba hutokana na lugha ya asili zenye muwasala wa kinasaba moja. Katika kubaini uhusiano huo Kondrak (2019) amependekeza kigezo cha sauti mrejeo chini ya kanuni ya mabadiliko ya sauti zinazojirejea katika maneno yanayofanana. Kiujumla kipengele hiki kinaaminika kama njia thabiti ya kuchunguza maneno mnasaba hasa kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu za kihistoria za lugha ya asili. Hivyo basi maneno ya lugha mbili au zaidi hulinganishwa kwa kuangaliwa sauti zinazojirejea baina ya lugha zinazohusiana na kuchukuliwa kama ushahidi thabiti wa maneno mnasaba. Akifafanua zaidi, Kondrak anaeleza kuwa maneno yenye mfanano wa sauti hutoa ushahidi thabiti kwamba lugha fulani zina asili ya pamoja na hivyo bila kumbukumbu za maandishi, ushahidi huu ndio msingi wa kuunda historia ya familia za lugha. Uchunguzi wa makala hii umebaini sauti mrejeo zenye kutafautiana katika maneno mnasaba kama inavyobainishwa katika maelezo yafuatayo:

Sauti Mrejeo katika Maneno Mnasaba

Katika baadhi ya mazingira, kuna kurejeleana kwa sauti mbalimbali baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi ambapo sauti mbili tafauti baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi hujitokeza bila kubadili maana ya neno. Muktadha huo hubainisha maneno mnasaba baina ya lahaja hizi mbili na kuthibitisha uhusiano na uasili wa kihistoria baina ya lahaja hizo mbili kama inavyojitokeza katika data zifuatazo:

Data Na.1: Sauti Mrejeo /d/ na /l/

Inapojitokeza sauti /d/ katika Kimakunduchi katika muktadha huo huo wa neno bila kubadili maana sauti /l/ hujitokeza katika Kitumbatu. Mfano:

Kiswahili	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
dimbwi	limbu	dimbu
tononoka	lunduka	dunduka
dema	lema	dema
dimba	limba	dimba
kidevu	kilevu	kidevu
mdomo	mlomo	mdomo

Muktadha huu wa sauti mrejeo baina ya sauti /d/ na /l/ katika Kimakunduchi na Kitumbatu ulizungumziwa na Nurse na Hinnebusch (1991) ambapo walibainisha sauti hizo zinavyorejeana mfano; dipa > lipa na dimba > limba.

Data Na. 2: Sauti Mrejeo /ʎ/ na /l/

Katika Kitumbatu kuna sauti ya kitambaza cha mdomo meno /ʎ/ ambacho hakimo katika Kimakunduchi. Hivyo inapotokea Kitumbatu kutumia sauti [ʎ] katika neno hilo hilo Kimakunduchi hutumia kitambaza cha ufizi [l]. Mpishano huu wa sauti bila kubadili maana unathibitisha maneno mnasaba baina ya lahaja hizo. Kama inavyojitokeza katika data zifuatazo:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
lala	ʎaʎa	lala
tazama	ʎola	lola
amka	ʎamka	lamka

Maelezo na data yetu hapo juu inatuonesha maneno mnasaba ambapo sauti [ʎ] na /l/ ni sauti zinazorejeana katika umbo moja la neno ambalo halibadiliki maana.

Muktadha wa sauti /ʎ/ na /l/ ulielezwa pia na Nurse na Hinnebusch (1991; 1993) ambapo alisema inapojitokeza sauti /ʎ/ katika Kitumbatu, katika mazingira yale yale sauti hiyo hukosekana katika Kimakunduchi. Mfano:

Data Na. 3:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
Pua	puʎa	pua
Mvua	vuʎa	vua
Koo	koʎo	koo
Uongo	uʎongo	uongo
Zaa	vyaʎa	vyaa

Njaa	njaλa	njaa
Mguu	mguλu	mguu

Kwa mujibu wa Nurse na Hinnebusch (1991) yamejitokeza kutokana na Kitumbatu kutokuwa na mfumo wa mfuatano wa irabu mwishoni mwa neno. Akifafanua zaidi anasema kuwa maneno mnasaba yaliyoainishwa kupitia kwenye data ya hapo juu yalijitokeza kupitia lugha za mbalimbali za Kibantu. Mfano neno **pua** (kiswahili), **pʰula** katika (Chonyi, Giriyama, Rabai, Segeju), **mpuła** (Chimwiini), **múla** (Mwani) na **mula** (Maraba).

Kama kwamba haitoshi, Swadesh (1934) anasema kwamba iwapo tutakuta tofauti ya matamshi ya neno lile lile moja (pasipo tofauti ya maana), basi ichukuliwe kwamba zinaonesha namna kadhaa tu za mkengeuko (unaokubalika) wa vijenzi vya fonimu. Maelezo ya Swadesh pamoja na kuwa hakutaja moja kwa moja dhana ya sauti mrejeo na maneno mnasaba, yanatuonesha kuwa msamiati mmoja wenye maana sawa inayotafautiana kimatamshi tu. Hali hii hapana shaka inaonesha uhusiano wa kinasaba wa lugha au lahaja hizo kama inavyobainishwa katika data zifuatazo:

Data Na. 4:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
Asubuhi	λunju	unju
Ubavu	λubavu	ubavu

Omba	λomba	omba
Ulimi	λulimi	ulimi
Uzi	λuzi	uzi
Umwa	λumwa	umwa
Uso	λuso	uso

Data Na. 5: Sauti Mrejeo /w/ na /j/

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
sisi	suye	suwe
yeye	nyuye	nyuwe
kifefe	kifyefye	kifwefwe

Sauti Mrejeo /k/ na /y/

Tukiangalia kijuujuu katika muktadha wa umbo tunaweza kusema kwamba sauti [k] na sauti [y] zimetofautiana sana na hivyo kurejeana kwa sauti hizi katika msamiati wa aina moja bila shaka ilitegemewa kuwa pengine maana zingekuwa ni tofauti. Hata hivyo muktadha kama huu katika Kitumbatu na Kimakunduchi ni tofauti kwa vile pamoja na sauti hizo kutofautiana lakini bado maana ya msamiati ni ile ile. Hali hii inaonesha kuwa haya ni maneno mnasaba inavyoonekana katika data ifuatayo:

Data Na. 6:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
ota	yota	koota
oga	yoga	koga
ogelea	yogeleza	kogelela

Sauti Mrejeo /py/ na /t/

Katika baadhi ya mazingira katika Kitumbatu na Kimakunduchi kuna tafauti ya matamshi ambapo sauti [py] na sauti [t] hurejeana kutokana na kujitokeza kwenye msamiati mmoja wenye maana moja na mazingira sawa ya ujitokezaji. Zingatia data ifuatayo:

Data Na. 7:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
ota	yota	koota
oga	yoga	koga
ogelea	yogeleza	kogelela

Ifahamike kwamba sauti /py/ haijaanishwa katika jadweli la kimataifa la sauti lakini kiuhalisia sauti hii ipo na hutumika katika lugha mbalimbali za Kibantu kama anavyoeleza Chomsky na Halle (1968) na kunukuliwa na Massamba (2012) pamoja na Iddi (2012 na 2018). Kutobadilika kwa maana kwa maneno yaliyoainishwa hapo juu katika jadweli inayoonesha kuwa haya ni maneno mnasaba ambapo tafauti ya matamshi haijasababisha mabadiliko kutokana na uhusiano wa asili wa kinasaba wa kuwa na mamelugha moja kwa lahaja hizi.

Data Na. 8: Sauti Mrejeo /g/ na /ɠ/

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
nyeupe	ɠelupe	geupe
nyeusi	ɠilufi	geusi
Ndege mnyama	ɠegemea	gegemea
chakua	ɠuɠunda	gugunda

Mabadiliko ya sauti hayakusababisha kubadilika kwa maana jambo ambalo linaonesha sauti mrejeo katika maneno hayo kama ilivyojitokeza katika mifano yetu hapo juu na kutubainishia kuwa haya ni maneno mnasaba.

Sauti Mrejeo /p/ na /v/

Wakizungumzia kuhusu sauti hizi, Nurse na Hinnerbusch (1991) hawakuhusisha moja kwa moja na Kitumbatu bali walihusisha na Kimakunduchi na kubainisha kuwa inapotokea sauti [p] katika Kiswahili Sanifu, sauti hiyo hugeuka na kuwa [v] katika Kimakunduchi. Katika maelezo yao wanasema kuwa mabadiliko haya si ya bahati tu bali yanatokana na sababu za kijiografia. Pamoja na hayo, lahaja hizi zinahusiana

kihistoria na hivyo sauti zake zinarejeana ambapo mpishano wa sauti hizi katika msamiati hauathiri maana. Kujitokeza kwa sauti hizi katika mazingira ya aina moja kwenye lahaja mbili; Kitumbatu na Kimakunduchi, bila ya shaka kunaonesha uhusiano wa kinasaba uliopo baina yao. Hali kama hii inajitokeza katika; lahaja hizi mbili, kwa baadhi ya muktadha, inapotamkwa sauti [p] katika Kitumbatu, sauti hiyo katika Kimakunduchi hutamkwa [v] jambo linaloonesha kuwa haya ni maneno mnasaba. Kwa mfano:

Data Na. 9:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
pika	pika	vika
peleka	peleka	veleka
pumua	pumua	vumua
papasa	papasa	vavasa
popote	poposi	Vovosi
puliza	puliza	Vuliza
hapa	pano	vano

Wakizungumzia kuhusu sauti hizi, Nurse na Hinnerbusch (1991) hawakuhusisha moja kwa moja na Kitumbatu bali walihusiha na Kimakunduchi na kubainisha kuwa inapotokea sauti [p] katika Kiswahili Sanifu, sauti hiyo hugeuka na kuwa [v] katika Kimakunduchi. Katika maelezo yao wanasema kuwa mabadiliko haya si ya bahati tu bali yanatokana na sababu za kijiografia. Pamoja na hayo, lahaja hizi zinahusiana kihistoria na hivyo sauti zake zinarejeana ambapo mpishano wa sauti hizi katika msamiati hauathiri maana. Kujitokeza kwa sauti hizi katika mazingira ya aina moja kwenye lahaja mbili; Kitumbatu na Kimakunduchi, bila ya shaka kunaonesha uhusiano wa kinasaba uliopo baina yao.

Sauti Mrejeo /t/ na sauti /ʧ/

Katika Kimakunduchi kwenye baadhi ya mazingira sauti /t/ na /ʧ/ hurejeana. Muktadha huu hubainisha uhusiano wa kihistoria wa asili unaotokana na mamelugha moja ambapo sauti mrejeo pia zimejitokeza katika matumizi ya wakati ujao kama inavyojitokeza katika data ifuatayo:

Data Na. 10:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
unataka	kunataka	kunachaka
utakwenda	kutakwenda	kuchakwenda
watasoma	watasoma	wachasoma
watapika	watavika	wachavika
nitakula	nitakulya	nichakulya
tanua	tanula	chanua
taka	taka	chaka
unataka	kunataka	kunachaka

Mbali na hayo, muktadha wa kurejeana kwa sauti [ʧ] na [t] kumejitokeza pia katika lahaja za Kitikuu, Kipate na Kisiu (Nurse na Hinnebusch, 1991). Kama kwamba haitoshi, sauti mrejeo **[ʧ] na [s]** zinazoainisha maneno mnasaba pia zinajitokeza katika njeo ya wakati ujao nafsi ya kwanza kama inavyoonekana katika data ifuatayo:

Data Na. 11:

Kiswahili Sanifu	Kitumbatu	Kimakunduchi
nitavaa	savala	chavwaa
nitakupa	sakuka	chakuka
nitakubali	sadumba	chadumba
nitapika	nitapika	chavika
nitakuleteya	sakujisiya	chakujisiya

Data Na.11 inatuonesha kwamba sauti zinarejeana katika mazingira tafauti bila kubadili maana ya neno. Juma (2019) anasema kuwa katika Isimu-historia na Linganishi, sauti mrejeo ni hali ya sauti katika maneno mnasaba kurejea kwenye kitu kile kile kimoja hata kama sauti hizo zinatofautiana kimaumbo. Katika data yetu tunabaini kuwa sauti fulani inaweza kupatikana katika Kitumbatu lakini sauti hiyo isipatikane katika Kimakunduchi katika mazingira sawa.

Data Na. 12: Maneno Mnasaba yenye Sauti mbalimbali

Kiswahili Sanifu	Kitumbatu	Kimakunduchi
yeye	veye	yeye
nywele	nywili	nywele
chuo	kyuo	chuo
majani	magani	majani
wao	veo	wao
rafiki	rafiki	afiki
ondoka	lawa	yawa
harusi	harusi	hausi

chelewa	chelewa	chelewa

Data Na.12 inaonesha kwamba mfanano wa maneno mnasaba baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi ambao unatokana na ukweli kwamba lahaja hizi zina uhusiano wa kiasili. Hivyo tofauti ndogo ndogo zinazojitokeza husababishwa na mwachano wa lahaja hizi kijiografia.

Maneno Mnasaba yenye Maumbo Sawa

Katika kufafanua maneno mnasaba Kondrak (2019) anasema kuwa maneno kutoka lugha mbili au zaidi zenye kutokana na mamelugha moja, maumbo yake ya maneno pamoja na maana huweza kufanana. Hii ni kwa sababu lugha hizo tangu awali kuwa na asili moja. Kwa maneno mengine, pamoja na kutumika neno hilo katika lugha tafauti lakini neno hilo kiasili lilikuwa ni moja. Mfanano huo unadhirisha familia ya lugha moja inayotumika katika maeneo tafauti. Hali hii inathibitika katika Kitumbatu na Kimakunduchi kama inavyoonekana kwenye data ifuatayo:

Data Na.13:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
jino	gino	gino
bahari	pwaa	pwaa
mvua	vula	vua
anguka	(ku)gwa	(ku)gwa
nchi	chi	chi
nzi	zi	zi
goti	futi	futi
titi	ziwa	ziwa

uvuvi	mavuvi	mavuvi
jicho	dicho	dicho
mgonjwa	mwele	mwele
tazama	lola	lola

Data iliyowasilisha ni ya msamiati wa msingi. Kupitia data Na.13, imedhihirika kwamba hakuna mabadiliko ya sauti ambayo yangesababisha sauti hizo kurejeana. Vile vile, kufanana kwa msamiti wa msingi unathibitisha uhusiano wa kinasaba uliopo katika Kitumbatu na Kimakunduchi jambo linaloonesha kuwa lahaja hizi zinatokana na mamelugha moja

Kama kwamba haitoshi, moja katika sifa ya lugha zenye asili, chimbuko na mamelugha moja ambazo zinawekwa katika kundi moja la familia ni msamiati wa msingi. Kigezo hiki ni imara kwa vile si aghalabu kukumbwa na mabadiliko. Hivyo basi, kwa kiasi kikubwa msamiati wake wa msingi hufanana na kusaidia kuthibitisha unasaba uliopo baina ya lugha au lahaja hizo. Msamiati wa msingi ni ule ambao unahusu vitu vya kawaida katika mazingira ya wazungumzaji wa lugha zinazohusika, vitu hivyo ni pamoja na majina ya sehemu za mwili, vitu vya maumbile na shughuli za kila siku za jamii zinazohusika Massamba (2017). Msamiati huo huweza kuhimili vishindo vya mabadiliko katika jamii jambo ambalo mara nyingi msamiati huo hubakia katika uasili wake kama inavyodhirika kwa Kitumbatu na Kimakunduchi katika data ifuatayo:

Data Na.14:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
macho	macho	macho
meno	meno	meno
milima	milima	milima

nyuso	nyuso	nyuso
mbingu	mbingu	mbingu
kichwa	kichwa	kichwa
mito	mito	mito
jua	jua	jua

Data Na.14 iliyowasilishwa inaonesha kuna mfanano wa msamiati wa msingi baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi. Mfanano huo unatokana na ukweli kwamba lahaja hizi zina uhusiano wa kimnasaba kutoka mamelugha ni moja.

Maneno Yanayotafautiana Maumbo

Kondrak (2019) anaeleza kuwa lugha zenye asili moja mara nyingi maneno yao hufanana kwa sauti na maana. Hata hivyo, baada ya muda mrefu kupita maneno hayo huweza kupata umbo tofauti kabisa la kifonetiki. Kwa mfano, Kiingereza *hundred*, Kifaransa *cent*, na Kipolandi *sto*. Maneno yote haya yametokana na lugha za Kihindi-Ulaya. Ama kwa hakika, kutokana na mabadiliko mbalimbali ya lugha yaliyojitokeza ulimwenguni, baada ya karne nyingi kupita, maneno mnasaba katika Kitumbatu na Kimakunduchi nayo yameweza kuathirika na kupata mabadiliko. Jambo hilo liliweza kusababisha kutafautiana kwa maumbo. Hata hivyo, pamoja na mabadiliko hayo maana za maneno zinalingana na kufanana kama inavyoonekana katika data ifuatayo:

Data Na.15:

Kiswahili Sanifu	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**
kipande cha nazi	kihanu	cheua
zungumza	ronga	choweya

baridi	pupwe	mande
njaa	njal'a	ujoma
kojoa	kwinyaya	baua
tafuta	tafuta	wapa
mtoto	mwana	mwanakele

Kuna maneno yenye tafauti za kimaumbo baina ya Kitumbatu na Kimakuduchi. Ingawa maumbo ya maneno hayo yanatafautiana lakini maneno hayo yana maana moja kisemantiki. Hali hii kama ilivyokwishaelezwa awali kuwa inatokana na mabadiliko ya muda mrefu. Kwa mujibu wa Kondrak mabadiliko haya yaliyosababisha tafauti za kimaumbo yanatokana na mchakato wa kihistoria wa lugha ambapo mabadiliko tafauti kutokana na maingiliano na muachano wa muda mrefu.

Hitimisho

Makala hii imechambua maneno mnasaba kwa kupitia sauti mrejeo baina ya Kimakunduchi na Kitumbatu. Makala imebaini sauti mrejeo tafauti tafauti baina ya maneno yanayoelezea kitu kimoja. Aidha, pamoja na kutafautiana kwa sauti katika maneno hayo lakini maana ni ile ile haibadiliki.

Kwa ujumla, pamoja na sauti hizo kutofautiana kwa kutofanana kiumbo lakini zimethibitika kwamba zinarejeana na hivyo maana katika msamiati wake haibadiliki. Muktadha huu unatuonesha kwamba sauti hizi hazijarejeana kwa bahati nasibu tu, bali kuna uhusiano baina ya sauti hizo kama zilivyochambuliwa katika maelezo yetu.

Kwa upande mwengine makala imeainisha maneno ambayo yametafautiana kiumbo lakini maana zinalingana. Matokeo haya yanaonesha kwamba, tafauti zote zilizojitokeza inaweza kuwa zimesababishwa na kutengana kwa lahaja hizi kwa muda mrefu sana na hivyo kupatikana sauti mrejeo baina yao. Pia mwingiliano wa jamii tafauti tafauti ambazo huenda zimesababisha mabadiliko katika baadhi ya msamiati ama kwa kufuata matamshi au kwa sababu ya maneno ya mkopo yaliyoingia

katika lahaja hizi. Uhakiki wa data katika makala hii umeonesha kwamba sauti zote ambazo zinapatikana katika Kimakunduchi zinapatikana pia katika Kitumbatu isipokuwa kwa sauti mbili tu; kitambaza cha mdomo na meno [λ] ambacho kinapatikana katika Kitumbatu pekee. Hata hivyo pamoja na kufanana kwa mfumo wa sauti hizo baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi, matumizi ya sauti hizo hutofautiana katika baadhi ya mazingira na kusababisha sauti hizo kurejeana kwa sifa zake kuu bila kuathiri maana kama ilivyobainishwa katika uchambuzi wa makala hii.

Pamoja na tafiti mbalimbali kufanyika kuhusiana na maneno mnasaba na sauti mrejeo imedhihirika kwamba tafiti katika lugha ya Kiswahili na lahaja zake pamoja na lugha za Kibantu bado zinahitajika. Kufanyika kwa tafiti hizo kutasaidia kuimarisha hoja zilizopo za wataalamu kuhusiana na uhusiano wa lugha ya Kiswahili na lugha na Kibantu na pia kuonesha mipaka iliyopo ya kiunasaba na kihistoria ya lugha hizo. Hii ni kwa sababu, inaaminika kwamba lugha za Kibantu katika Bara la Afrika zina uhusiano na chimbuko la asili moja. Pia, kwa vile Bara la Afrika lina lugha nyingi, tafiti zitaweza kujumuisha lugha mbalimbali za Kiafrika na kubainisha uhusiano wa asili wa lugha hizo, mamelugha zao pamoja na historia ya familia za lugha za Kiafrika kwa ujumla.

Marejeleo

Anttila, R. (1972). *An introduction to historical and comparative linguistics*. New York, NY: Macmillan.

Batsuren, K., Bella, G., & Giunchiglia, F. (2019). CogNet: A large-scale cognate database. In A. Korhonen, D. Traum, & L. Màrquez (Eds.), *Proceedings of the 57th Annual Meeting of the Association for Computational Linguistics* (pp. 3136–3145). Florence, Italy: Association for Computational Linguistics. https://doi.org/10.18653/v1/P19-1302

Brown, C. H., Holman, E. W., & Wichmann, S. (2013). Sound correspondences in the world's languages. *Language, 89*(1), 4–29.

Chamizo Domínguez, P. J. (2008). *Semantics and pragmatics of false friends*. New York, NY: Routledge. https://doi.org/10.4324/9780203941775

Chomsky, N. (1967). Some general properties of phonological rules. *Language, 43*(1), 102–128. https://doi.org/10.2307/411387

Chomsky, N., & Halle, M. (1968). *The sound pattern of English*. New York, NY: Harper & Row.

Clackson, J. (2007). *Indo-European linguistics: An introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

de Groot, A. M. B. (2011). *Language and cognition in bilinguals and multilinguals: An introduction*. New York, NY: Psychology Press. https://doi.org/10.4324/9780203841228

Dyen, I., Kruskal, J. B., & Black, P. (1992). *An Indo-European classification: A lexicostatistical experiment*. Philadelphia, PA: American Philosophical Society.

Frunza, O. M. (2008). *Cognates, false friends, and partial cognates*. Saarbrücken: VDM Verlag.

Howatt, A. P. R., & Smith, R. (Eds.). (2000). *Foundations of foreign language teaching: Nineteenth-century innovators* (6 vols.). London: Routledge.

Iddi, Z. A. (2011). *Phonological processes in Kimakunduchi dialect* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Iddi, Z. A. (2017). *Ulinganishi wa kiisimu baina ya Kitumbatu na Kimakunduchi* (Tasnifu ya uzamivu ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.

Igoa, J. M., & García Albea, J. E. (1992). Lexical access in bilinguals: Effects of cognate status and language context. *Journal of Memory and Language, 34*(5), 476–495.

Jones, W. (1786). The third anniversary discourse, delivered to the Asiatic Society, on the Hindus. *Asiatic Researches, 1*, 415–431.

Kondrak, G. (2003). Identifying complex sound correspondences in bilingual wordlists. In A. Gelbukh (Ed.), *Computational linguistics and intelligent text processing: Proceedings of CICLing 2003* (pp. 432–443). Berlin: Springer. https://doi.org/10.1007/3-540-36456-0_46

Kondrak, G. (2009). Identification of cognates and recurrent sound correspondences in word lists. *Traitement Automatique des Langues, 50*(2), 201–235.

Kroonen, G. (2013). *Etymological dictionary of Proto-Germanic*. Leiden: Brill.

List, J.-M., Greenhill, S. J., & Gray, R. D. (2017). The potential of automatic word comparison for historical linguistics. *PLOS ONE, 12*(1), Article e0170046. https://doi.org/10.1371/journal.pone.0170046

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo ya nadharia ya fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2012). *Misingi ya fonolojia*. Dar es Salaam: TATAKI.

Meillet, A. (1954). *La méthode comparative en linguistique historique*. Paris: Honoré Champion.

Nurse, D., & Hinnebusch, T. J. (1993). *Swahili and Sabaki: A linguistic history* (University of California Publications in Linguistics, Vol. 121). Berkeley, CA: University of California Press.

St Arnaud, A., Beck, D., & Kondrak, G. (2017). Identifying cognate sets across dictionaries of related languages. In M. Palmer, R. Hwa, & S. Riedel (Eds.), *Proceedings of the 2017 Conference on Empirical Methods in Natural Language Processing* (pp. 2519–2528). Copenhagen, Denmark: Association for Computational Linguistics. https://doi.org/10.18653/v1/D17-1267.

Swadesh, M. (1971). The Origin and Diversification of Language. Ed. Post Mortem by Joel Sherzer. *Contains Final 100 –Words List on p. 283*. Chicago: Aldine.

Swadesh, M. (1934). *The phonemic principle*. Language, 10(2), 117–129.